

Mbunge wa jimbo la katavi ambaye pia ni waziri wa wizara ya maji eng. Isack Aloyce Kamwelwe amewataka baadhi ya walimu wenye tabia ya kupuuzia mambo ya muhimu kwa kisingizio cha kutowajibika wenyewe kuacha tabia hiyo mara moja.

Akiongea na walimu kwenye tafrija fupi ya kuzipongeza shule za msingi zote kwa kuifanya Halmashauri ya wilaya ya Mlele kushika namba sita kitaifa, namba moja kikanda na kimkoa katika mtihani wa darasa la saba mwaka 2017.

cut

Amesema kuwa kila mwalimu awe tayari katika kutekeleza jukumu lake la kufundisha katika mazingira yeyote ili kuendelea kuinua kiwango cha elimu katika Halmashauri.

Aidha Mh, Kamwlwe ameelezea mpango mkakati wa kuhakikisha kila kata katika Halmashauri inakuwa na sekondari moja yenye kidato cha kwanza hadi cha nne, ambapo tayari Halmashauri imekwisha sajiri sekondari tatu katika kata za Inyonga, Utende na Ilela.

Pia ameongeza kusema kuwa halmashauri inampango wa kuwa na sekondari mbili kwa kidato cha tano na sita ikiwa tayari imekwisha kamilisha ujenzi wa miundombinu na usajili wa shule ya sekondari Inyonga kwa kidato cha kwanza hadi cha sita.

Huku kata za ilunde na Nsenkwa zikiendelea na ujezi wa miundombinu ya shule, kata ya Kamsisi ikiwa kwenye mpango wa kuanza kujenga miundombinu kufikia mwakani.

Cut

Halmashauri ya wilaya ya mlele ina jumla ya shule za msingi 13 zilizosajiliwa shule 3 ni za sekondari kidato cha kwanza hadi cha nne na shule moja ya kidato cha kwanza hadi cha sita.